



**CATHOLIC DIOCESE OF MOSHI**  
**ST. PAMACHIUS INCLUSIVE SECONDARY SCHOOL**  
P. O. BOX 1303  
**MOSHI – TANZANIA**  
st.pamachiusinclusive2019@gmail.com

**SHERIA, TARATIBU NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

**1. UTANGULIZI**

Taratibu hizi zinawahu su wote wanaosoma katika Shule ya Sekondari St. Pamachius Inclusive.

Lengo la sheria hizi ni kuweka utaratibu na mpangilio wa mahusiano ya wanafunzi na walezi wao katika kanuni zinazoheshimika na wote, ili mwanafunzi afikie weze kufaulu vema na kufikia malengo yake. Upo usemi usemao “Power without control is useless”. Elimu bora inampa nwanafunzi maarifa (“Power”). Maadili mema yanampa mwanafunzi udhibiti bora wa malengo na maisha yake (Control). Kwa kutii sheria hizi tutashiriki utume wa Jimbo Katoliki Moshi (Mwenye Shule) wa kujenga jamii adilifu ya Kitanzania yenye kuunganisha maarifa na nidhamu ya maisha. Hivyo, sheria hizi zinawahu su wote pasipo upendeleo wo wote.

Shule hii ni mali ya Jimbo Katoliki Moshi. Ni dhahiri kuwa malezi na maadili yanayotolewa katika Shule hii yatakuwa na ladha ya mafundisho sahihi ya Kanisa Katoliki.

Pamoja na Sheria za Shule zinazotambulishwa hapa, Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote iliyopo, inayotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Sera ya Elimu ya Wizara ya Elimu, Sera ya Elimu ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania na Sera ya Elimu Jimbo Katoliki Mosh. Hivyo ni muhimu kwa Mwanafunzi kutambua upekee wa nafasi aliyopata kusoma katika Shule yetu.

Malezi ya wanafunzi kitaaluma, kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya Wanafunzi, Waalimu na Wazazi. Uongozi wa Shule ya Sekondari St. Pamachius Inclusive unatoa rai kwa Wazazi na Walezi kuunganisha jitihada zao katika malezi ya watoto. Lengo letu liwe ni kuhakikisha malengo mema ya shule ya kuwawezesha watoto kufaulu kwa kiwango cha juu, yanafikiwa kwa ufanisi mkubwa.

Kwa kuzingatia wajibu huo, Mzazi / Mlezi wa mtoto asome sheria hizi na kuzielewa. Kisha mwanafunzi azisome na akiri mbele ya mzazi kuwa yuko tayari kufuata sheria hizi katika tamko lililoambatishwa na maeleo haya ya kuijunga na shule yetu. Mungu aliye asili ya wema wote, awawezeshe wanafunzi wote kuzingatia utaratibu huu kwa sifa na utukufu wake. Amina.

**2. MAZOEYA YA KAWAIDA SHULENI**

Wakati wote wa masomo na malezi, mwanafunzi anategemewa:

- 2.1 Kufuata ratiba ya shule kwa umakini
- 2.2 Kuwahi kila mahali
- 2.3 Kupangilia na kutumia muda wake vema
- 2.4 Kuonesha tabia njema kwa maneno na matendo yake maadilifu.
- 2.5 Kuwa na bidii katika masomo
- 2.6 Kuwajibika katika shughuli nyingine atakazokabidhiwa.
- 2.7 Ushirikiano na wanafunzi wenzake na Waalimu wote
- 2.8 Kuwaheshimu watu wote.
- 2.9 Kutunza usafi binafsi na wa mazingira yanayomzunguka
- 2.10 Kujali na kutunza mali za shule
- 2.11 Kutumia vitu alivyopewa na wazazi (fedha na vifaa mali binafsi) kwa umakini
- 2.12 Awepo ndani ya eneo la shule wakati wote wa mhula wa masomo.
- 2.13 Kuvaa sare ya Shule wakati wote

2.14 Kutumia lugha zinazoruhusiwa shuleni (Lugha ya Alama ya Tanzania na Kiingereza)

### **3. Mambo Yanayokatazwa Katika Shule Yetu (Mwiko)**

Wakati wote awapo shuleni, inakatazwa, na ni marufuku kwa Mwanafunzi:

- 3.1 Kumiliki
- 3.2 Kutumia simu pasipo ruhusa
- 3.3 Kutoroka
- 3.4 Kuiba
- 3.5 Kulewa
- 3.6 Kuwa mvivu
- 3.7 Kuwa na mahusiano yo yote ya kimapenzi
- 3.8 Kuvuta sigara
- 3.9 Kutumia madawa ya kulevya
- 3.10 Kubagua wengine kwa misingi ya Jinsia, Ulemavu, au kigezo kingine cho chote
- 3.11 Kutembelea nyumba za wahudumu wa Shule
- 3.12 Kutoava sara ya shule kadiri ilivyoagizwa

### **4. Makosa Yatakayomfanya Mwanafunzi Kufukuzwa Shule Mara Moja**

Shule inatambua uwepo wa miongozo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Jimbo Katoliki Moshi inayoelekeza adhabu mbalimbali, ikiwemo kufukuzwa shule, kutokana na makosa kadhaa. Pamoja na yaliyotajwa katika miongozo hiyo, Mwanafunzi atakayebainika katika mojawapo kati ya mambo yafuatayo, atafukuzwa shule mara moja.

- i. Kuwa mjauzito
- ii. Kumpa mwanafunzi / mtu mwengine ujauzito
- iii. Kutoa mimba
- iv. Kushiriki / kushawishi / kufundisha / kuhimiza mwengine kutoa mimba
- v. Mahusiano ya kimapenzi
- vi. Ubakaji
- vii. Ulawiti
- viii. Wizi
- ix. Ulevi (wa Pombe au Madawa ya Kulevya)
- x. Kupigana
- xi. Utoro
- xii. Unyanyapaa
- xiii. Matumizi ya simu shuleni
- xiv. Kuoa au kuolewa [1] [SEP]
- xv. Kugoma
- xvi. Kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama shuleni

.....  
Pd. Patrick Asanterabi  
**MKUU WA SHULE**